TANGAZO LA SERIKALI Na. 284 la tarehe 19/03/2021

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Imetungwa chini ya vifungu vya 7(1) (u) na 16(1)

SHERIA NDOGO YA USHURU WA HUDUMA
YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA YA MWAKA 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri Wilaya ya Igunga za mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo: -

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Igunga;

"Hesabu" maana yake ni taarifa ya maandishi na au vielelezo vinavyoonesha taarifa za mapato ya mlipa ushuru, kwa lengo la kukokotoa ushuru wa huduma;

"Kipindi cha hesabu" maana yake ni kati ya miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka ambacho mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu zake;

"Mamlaka ya Mapato" Maana yake ni Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga pamoja na Afisa yeyote atakayetueuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mlipa Ushuru" maana yake ni kampuni au taasisi ya kibiashara, inayowajibika kulipa ushuru wa huduma chini ya sheria ndogo hii na itahusisha Mkurugenzi, Meneja au Afisa msimamizi wa taasisi ya kibiashara ambaye anapaswa kulipa ushuru wa huduma kwa niaba ya taasisi husika; na itahusisha mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara au anayepaswa kuwa leseni ya biashara kwa mujibu wa Sheria ya Leseni za Biashara;

Sura ya 208

"Mwaka wa hesabu" maana yake ni kipindi miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

"Mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote mwenye leseni ya biashara au anayepaswa kuwa na leseni ya biashara;

"Taasisi isiyo ya kibiashara" maana yake ni taasisi isiyo ya kiserikali au mtu ambaye anafanya shughuli za kujitolea kusaidia jamii katika maeneo ya elimu, afya, maji, miundombinu, kuondoa au kupunduza umaskini, kutoa huduma za kidini, au kusaidia watu walioathirika na majanga, bila malipo, au ambaye ana ushahidi wa maandishi kuhusu uamuzi wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kutambua taasisi hiyo au mtu huyo kama taasisi isiyo ya kibiashara au taaasisi ya kusaidia;

"Taasisi ya kibiashara" maana yake ni Kampuni, taasisi, tawi la kampuni au taasisi au asasi isiyo ya kiserikali, iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Makampuni au sheria ya majina ya kibiashara au ushirika, inayojishughulisha na shughuli za utafiti wa kibiashara, uzalishaji, usambazaji au uuzaji wa bidhaa, mazao au huduma.

"Ushuru" maana yake ni ushuru wa huduma;

"Ushuru wa huduma" maana yake ni malipo yanayolipwa na mlipa ushuru kwa Halmashauri kwa huduma za umma anazotumia kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, taasisi au kampuni, iliyoteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru wa huduma.

Utozaji wa Ushuru wa Huduma

3. - (1)Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kutoka kwa mlipa ushuru kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mapato ghafi ya mlipa ushuru, baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji kutokana na shughuli za kibiashara, ziwe za uzalishaji au usambazaji au uuzaji wa bidhaa au mazao au huduma ndani ya eneo la Halmashauri.

(2)Kifungu kidogo cha 1 hakitazihusu taasisi zisizo za kibiashara

Wajibu wa kulipa Ushuru

4. Utakuwa ni wajibu wa mlipa ushuru anayefanya shughuli zake ndani ya eneo la halmashauri, kulipa ushuru wa

huduma kwa halmashauri kila mwanzo wa mwaka wa kalenda.

Taratibu za kulipa Ushuru wa Huduma

5. - (1) Kila mlipa ushuru, atawasilisha hesabu za mapato yake kwa halmashauri ndani ya siku ishirini na moja tangu kuisha kwa kipindi cha hesabu.

(2) Mlipa ushuru atapaswa kulipa ushuru wa huduma ndani ya siku saba tangu tarehe ya kukokotolewa kwa ushuru kutokana hesabu sahihi za mapato yake aliyowasilisha.

(3) Mlipa Ushuru ambaye atashindwa kuwasilisha hesabu za mapato yake kwa wakati au ambaye kwa maoni ya Mkurugenzi au afisa muidhiniwa hesabu zitakazokuwa zimewasilishwa na mlipa ushuru zitaonekana kuwa na mapungufu kiasi cha kuathiri ukokotoaji wa ushuru sahihi, atapaswa kulipa ushuru wa huduma kwa viwango vilivyotajwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii pamoja na asilima kumi ya ushuru.

(4) Mkurugenzi anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu mlipa ushuru yeyote anayepaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kuwasilisha kwake taarifa ambazo zitatumiwa kusaidia kulipwa kwa ushuru.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

6. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri, kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini, kufanya ukaguzi wa vitabu au kufanya jambo lolote linalohusu ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii

Wakala

7. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii

Makosa

8. Itakuwa ni kosa kwa mlipa ushuru yeyote :–

a) kushindwa kuwasilisha hesabu sahihi za mapato yake;

b) kushindwa kulipa ushuru kwa wakati;

c) kushindwa kuwasilishwa nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa katika muda uliowekwa;

d) kushindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka anazopaswa kutunza kuhusu ushuru;

e) kufanya hesabu za uongo kwa kupunguza mapato

yake au ushuru isivyo halali;

f) kutoa taarifa za uongo kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri wajibu wake au wajibu wa mtu mwingine kuhusu ulipaji wa ushuru;
g) kuandaa au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa hesabu au kumbukumbu za uongo ambazo zinaweza kuathiri ukokotoaji wa ushuru;
h) kumzuia au kujaribu kumzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii;
i) kuharibu kwa makusudi au kwa uzembe taarifa au mfumo wa taarifa za hesabu;
j) kuharibu kwa makusudi au kwa uzembe vitendea kazi vya kukusanyia ushuru;
k) kukataa kupokea au kusaini uthibitisho wa kupokea hati, taarifa au notisi chini ya Sheria Ndogo hii, iliyoelekezwa kwake au mtu mwingine ambaye anafanya kazi ofisini mwake au anaishi nyumbani mwake;
l) kutenda jambo lolote kinyume na Sheria Ndogo hii.

Adhabu

9. Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa ushuru anaodaiwa na faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au atatumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyobainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA
(Limetungwa chini ya Kifungu cha 5(3)

VIWANGO VYA USHURU WA HUDUMA KWA ASIYEWASILISHA TAARIFA YA MAPATO

NA.	Ada ya Leseni ya Biashara(TSh.)	Ushuru wa Huduma kwa Mwaka (TSh)
1	5,000 – 7,999	20,000.00
2	8,000 – 9,999	30,000.00
3.	10,000 – 19,999	40,000.00
4.	20,000 – 29,999	50,000.00
5.	30,000 – 39,999	60,000.00
6.	40,000 – 49,999	80,000.00
7.	50,000 – 59,999	200,000.00
8.	60,000 – 69,999	250,000.00
9.	70,000 – 79,999	300,000.00
10	80,000 – 89,999	350,000.00
11.	90,000 – 99,999	400,000.00
12.	100,000 -119,999	500,000.00
13.	120,000 – 139,999	600,000.00
14.	140,000 – 159,999	650,000.00
15.	160,000 – 189,999	700,000.00
16.	190,000 – 219,999	750,000.00
17.	220,000 – 239,999	800,000.00
18.	240,000 – 269,999	850,000.00
19.	270,000 – 300,000	900,000.00
20.	300,001 – 350,000	950,000.00
21.	350,001 – 400,000	1,100,000.00
22.	400,001 – 450,000	1,200,000.00
23.	450,001 – 500,000	1,300,000.00
24.	500,001 – 550,000	1,400,000.00
25.	550,001 – 600,000	1,500,000.00
26.	600,001 – 650,000	1,600,000.00
27.	650,001 – 700,000	1,700,000.00
28.	700,001 – 750,000	1,800,000.00
29.	750,001 – 800,000	1,900,000.00
30.	800,001 – 850,000	2,000,000.00
31.	850,001 – 900,000	2,200,000.00
32.	900,001 – 950,000	2,400,000.00
33.	950,001,1,000,000	2,600,000.00

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA
(Limetungwa chini ya kifungu cha 10)

A. KUKIRI KOSA

Mimi…….……nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya……..……ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, kwamba mnamo tarehe…….mwezi……Mwaka……..nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha……cha Sheria ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru wa Huduma ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……..ya Mwezi……Mwaka…….

Jina……Saini…….…….

Mbele ya:

Jina……Cheo……..

Saini……..Tarehe……

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 30 mwezi Aprili, 2020 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na:-

REVOCATUS L.K.KUULI
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Igunga

PETER ONESMO MALODA
Mwenyekiti wa Halmashauri
Halmashauri ya Wilaya ya Igunga

NAKUBALI,

Dodoma
22 Februari 2021

SELEMANI S. JAFO (MB)
Waziri wa Nchi – OR- Tamisemi